

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE



12 JUNI, 2019

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 12 JUNI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**365. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katika kujenga Tanzania ya Viwanda Serikali imekuwa na mikakati ya muda mrefu:-

Je, ule mkakati wa Ofisi ya Rais TAMISEMI wa kujenga Viwanda 100 kwa kila Mkoa ni sehemu ya mkakati na umeainishwa kwenye Waraka gani wa Serikali ili kuwapa Wananchi rejea ya pamoja ya Kitaifa.

**366. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM
(MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mwaka 2019 kutafanyika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria:-

Je, Serikali ina mkakati gani unaoendelea katika maandalizi ya mchakato wa Uchaguzi huo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**367. MHESHIMIWA ALMAS ATHUMAN MAIGE
(TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Miaka iliyopita Serikali ilikuwa na nia ya kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika Shule za Msingi na za Upili:-

(a) Je, nini kilitokea kwa Serikali katika kutekeleza nia yake hiyo nzuri;

(b) Je, lini Serikali itaanza kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika Shule za

Msingi na za Upili ili kukuza uelewa wa Wanafunzi katika masomo yao.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

368. MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Wananchi wengi katika Kata za Fukayosi na Kiwangwa Bagamoyo wanalima Mananasi kwa wingi sana:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhusu kuwajengea Viwanda vya kuchakata zao hilo ili kuboresha kipato cha Wakulima hao.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

369. MHESHIMIWA YOSEPHER FERDINAND KOMBA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Nyumba za makazi pembezoni mwa reli Wilayani Muheza zimewekewa alama ya 'x' zikisubiri kubomolewa kwa kigezo cha kujenga kwenye eneo la reli wakati walipewa maeneo hayo kihalali na Serikali:-

Je, ni nini hatma ya Wananchi hao ambao wanaishi kwa mashaka.

370. MHESHIMIWA AJALI RASHID AKBAR (NEWALA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

- (a) Je, kipimo halisi cha barabara kuu ya lami ni kipi;
- (b) Je, upana kwenye Miji ipitayo barabara unafanana na eneo ambalo halina makazi;
- (c) Kama upana haufanani kwenye Miji na eneo la makazi Je, ni nini kipimo halisi.

WIZARA YA MADINI:

371. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJAB (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Serikali ilituma Wataalam wa Madini, Mazingira na Maji katika Kijiji cha Sakale Tarafa ya Amani kuangalia uwezekano kama uchimbaji wa Dhahabu unawezakana katika maeneo hayo:-

Je, Serikali imefikia uamuzi gani kuhusu suala hilo.

372. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-
Kampuni ya Mabangu ina Leseni ya utafiti wa Madini katika maeneo ya Nyakafara, Bukandwe na Kanegere Wilayani Mbogwe; Kampuni hiyo inafanya utafiti kwa kushirikiana na Kampuni nyingine ya *Resolute* lakini utafiti huo umechukua muda mrefu:-

(a) Je, ni lini Kampuni hizo zitafungua Mgodini katika eneo lao la utafiti;

(b) Kama Kampuni hizo zimeshindwa kuanzisha Mgodini; Je, Serikali iko tayari kuona uwezekano wa kuligawa eneo hilo kwa Wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Mbogwe.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

373. MHESHIMIWA MUNIRA MUSTAPHA KHATIB (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kumekuwa na biashara haramu za mitandao maarufu kama *Pyramid Schemes*. Biashara ambazo zimeshamiri sana Miji ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti biashara hizo ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa uchumi wa Taifa;
- (b) Je, ni Kampuni ngapi za aina hiyo ambazo zimeingia nchini na kupata kibali cha kuendesha biashara za aina hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**374. MHESHIMIWA ENG. CHRISTOPHER
KAJORO CHIZA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wafanyabiashara wa Wilaya ya Kakonko wanapenda kujisajili BRELA ili kurahisisha biashara zao na kulipa Kodi stahiki lakini wengi wanashindwa kufanya hivyo kwa kukosa Vitambulisho vya Taifa:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha zoezi la kutoa Vitambulisho vya Taifa ili Wananchi waweze kuvitumia katika shughuli za maendeleo;
- (b) Kuna Wananchi wanaokaa katika mipaka kati ya Tanzania na nchi nyingine; Je, Serikali imewawekea utaratibu gani wa kuwapa Vitambulisho Wananchi hao kwa haraka bila kuathiri malengo ya zoezi la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa.

DODOMA
12 JUNI, 2019

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE